

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO**

MKOA WA SINGIDA

Anuanii: "AFYA

Simu Na: 026-2502397

Fax Na: 026-2502360

E-mail: regionalhospital@singida.go.tz

Unapojibu tafadhalii taja:



HOSPITALI YA RUFAA MKOA

S.L.P. 104,

SINGIDA.

01/10/2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa Mkoaa wa Singida amepokea maagizo kutoka kwa Katibu Mkuu (AFYA) kuititia barua Kumb. Na. 120/356/02A/105 ya tarehe 15 Septemba 2021 ikimtaka kutekeleza mwongozo wa kuwapata Wauguzi Viongozi katika ngazi zote za huduma za Afya nchini.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa Mkoaa wa Singida anakaribisha maombi ya kazi ya **Muuguzi Kiongozi (Matron/ Patron)** wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoaa wa Singida kutoka kwa Wauguzi wenyewe sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi 1 kama ilivyobainishwa katika Tangazo hili.

1.0 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kutoa huduma na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa katika idara anayolongoza.
- ii. Kusimamia wataalam na watumishi waliochini yake na kuhakikisha kuwa wanatoa huduma bora kwa wateja wao.
- iii. Kuwajengea uwezo wataalan waliochini yake ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma.
- iv. Kufundisha watumishi na warafunzi kutoka kwenye vyuo mbalimbali, interns na residents.
- v. Kuhudhuria vikao vya menejimenti vitakavyoitishwa na Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa Mkoaa wa Singida na kutoa mchango na ushauri wa namna ya kuboresha huduma za Hospitali.
- vi. Kuitisha na kusirnamia vikao ya idara ya Uuguzi na kutoa taarifa ya matokeo ya vikao hivyo kwa Mganga Mfawidhi.
- vii. Kufanya tathmini ya utendaji wa watumishi walio chini yake na inapotokea nafasi apendekeze jina au majina ya watumishi wenyewe uwezo wa kuteuliwa kwenye nafasi mbalimbali kwa menejimenti ya Hospitali kwa ajili ya uteuzi.
- viii. Kusimamia vizuri rasilimali zote zilizoko chini ya idara yake na kuhakikisha kuwa hazipotei na zinatumika vizuri kama ilivyokusudiwa.
- ix. Pamoja na watumishi walipo katika idara yake ataandaa mpango kazi na bajeti na kuwasilisha kwenye menejimenti ya hospitali kwa ajili ya kutengeneza mpango kabambe wa hospitali.

- x. Ataandaa na kuwasilisha taarifa za robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima za utekelezaji katika idara yake na kuzwasilisha kwa menejimenti ya hospitali ili menejimenti iweze kuzifanyia kazi.
- xi. Atasimamia shughuli za maboresho ya hospitali.
- xii. Atafanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe mtumishi mwenye Shahada ya Uuguzi
- ii. Awe amesajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga la Tanzania (Registered with the Tanzania Nursing and Midwives Council)
- iii. Awe na uzoefu walau wa niaka 5 wa kufanya kazi ya Uongozi katika eneo la Uuguzi/ Afya
- iv. Awe ni mtumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

1.2 MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania.
- ii. Waombaji wote waambatisho cheti cha kuzaliwa
- iii. Waombaji wote waambatisho maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detail cv) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Viambatanisho hivyo vibanwe sawasawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.
 - Posdtgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificate.
 - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI kwa waliofika kidato cha VI.
 - Vyeti vya kitaaluma (Professional certificate from respective boards).
 - Leseni ya Uuguzi na Ukganga.
 - Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni landikwe jina kwa nyuma.
- v. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- vi. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 11.10.2021 saa 9:30 Alasisiri.
- vii. Aidha atakaewasilisha barua yake kwa njia ya mkono ahakikishe anasaini kitabu maalumu cha kupokea barua hizi masijala.
- viii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza na yatumwe kupitia anuanii l'uatayo:-

**Mganga Mfawidhi,
Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Singida,
S.L.P 104,
SINGIDA.**



Khashim J. Muliro
Afisa Uhusiano
Hospitali ya Rufaa Mkoa
SINGIDA

**K.H. MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA
SINGIDA**